# SHIWANGO PRE KCPE EVALUATION TEST

## DARASA LA NANE (8)

KISWAHILI Muda: **Saa 1 Dakika 40 Min**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Ni jambo la __1__ kwa mwanafunzi __2___na nidhamu, bidii, na uwajibikaji iwapo angetaka kufanikiwa.wanafunzi wanatakiwa __3__ na wenzao ili kuongezeana maarifa __4___ si kwa kupotoshana. Kamwe mwanafunzi yeyote yule, __5__ nafsini mwake __6__ anaweza kufanikiwa __7___ __8___ asiyejua upweke ni uvundo.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | A. | muhimu | B. | muhali | C. | hiari | D. | daharura |
| 2. | A. | kua | B. | kukuwa | C. | kuwa | D. | kutokua |
| 3. | A. | kutangamana | B. | kutengana | C. | kutengemaa | D. | kutanga |
| 4. | A. | na | B. | wala | C. | bali | D. | ilhali |
| 5. | A. | asidanganye | B. | asiidanganye | C. | asijidanganye | D. | usimdanganye |
| 6. | A. | kua | B. | yakuwa | C. | yakwamba | D. | kwamba |
| 7. | A. | Peke yake | B. | Pekee yake | C. | peke | D. | upekee |
| 8. | A. | kwani | B. | wepi | C. | nani | D. | mgani |

Kipepesi ni njia mojawapo ____9__ sana siku hizi ___10____ mawasiliano. Njia ____11 ___ hutumika zaidi offisini. ___12___ni kati ya matokeo ya maendeleo ya kiteknolojia ____13____ dunia kuwa duara ndogo ___ 14___ walimwengu huweza ____ 15____ kwa njia rahisi.

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | A. | zilizotumika | B. | zinazotunika | C. | inayotumika | D. | iliyotumika |
| 10. | A. | katika | B. | kuhusu | C. | Ndani ya | D. | Mbali na |
| 11. | A. | hiyo | B. | hizi | C. | hizo | D. | hii |
| 12. | A. | ama | B. | aidha | C. | na | D. | au |
| 13. | A. | iliyoiwezesha | B. | yaliyoliwezesha | C. | iliyoliwezesha | D. | yaliyoiwezesha |
| 14. | A. | ambayo | B. | ambao | C. | ambapo | D. | ambalo |
| 15. | A. | kuwasiliana | B. | kuwasilisha | C. | kuwasilishwa | D. | kuwasilishiana |

***Kuanzia swali la 16 hadi 30 chagua jibu lililo sahihi kulingana na maagizo***

16. Chagua kivumishi kiashiria katika sentensi hii
    Dukani pake ndipo alipomwona mgeni yule
    A. pake
    B. mgeni
    C. alipomwona
    D. yule
17. Jaza mapengo vilivyo
    Mwanabiashara huyo

alilipa________kwa mkopo alioutumia kama ______kuanzisha biashara yake.

A. Fidia/mtaji
B. Riba/tijara
C. Ridhaa/faida
D. Riba/duhuli

18. Kanusha sentensi ifuatayo
Njungu iliyonunuliwa iliuzwa tena

A. Njungu iliyonunuliwa iliuzwa tena
B. Njungu iliyonunuliwa haikuuzwa tena
C. Njungu isiyonunuliwa haijauzwa tena
D. Njungu isiyonunuliwa haikuuzwa tena

19. Jengo la kufanya utafiti wa kisayansi huitwa

A. maabara
B. makavazi
C. handanki
D. maabadi

20. Ipi siyo sauti ghuna

A. t
B. g
C. v
D. b

21. Sentensi "Juma ni kinyonga"imetumia tamathali ipi?

A. Msemo
B. tashbihi
C. istiara
D. nahau

22. Homa ya kurudiarudia huitwaje

A. Kichemsho
B. Kidingapopo
C. Kifuaduro
D. kikohozi

23. Kipindi upepo unapovuma kutokea kusini huitwa

A. Matlai
B. kifuko
C. kusi
D. chaka

24. Chagua kifungu sahihi kukamilisha sentensi
alikitumia kisu _______ makali kuukata mkate_____

A. chenye/wenye
B. chenyewe/wenye
C. chenye/wenyewe
D. yenye/wenyewe

25. Mazingira ,machozi na mate ni nomino katika ngeli ya

A. YA-YA
B. I-ZI
C. LI-YA
D. U-YA

26. Kitenzi nawa katika kauli ya kutendesha ni

A. Nawika
B. Nawia
C. Navya
D. nawisha

27. Anayesimamia na kuidhinisha matumizi mazuri ya fedha katika shirika huitwa

A. Msarifu
B. Mhazili
C. Mhasibu
D. katikiro

28. Ipi si nomino ya dhahania

A. umati
B. usingizi
C. hasira
D. wema

29. Akisami $^{1}/_{7}$ ni

A. theludi

B. subui
C. sudusi
D. khumusi

30. Orodha ipi ya maneno iliyopangika vizuri kulingana na kamusi
A. somo,sononeka,shamrashamra,s aftahi
B. mamlaka,mamia,maliwazo,man dhari
C. kionjamchuzi,kipaimara,kipandi kizo,kipimajoto
D. urafiki,uwaziri,uvumbuzi,uraia

***soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40***

Ni jambo la kuvunja moyo kwa vile visa vingi vya kuvunja sheria vinavyozidi kuongezeka. Hali hii imeshuhudiwa sana katika mitaa yetu ya mabanda hata ile ya kifahari. Wahuni wanashiriki katika visa hivi bila kujali madhara wala maafa wanayosababisha. Wanastahili kuwa watu kuenga kabla ya kujenga. Hatukatai kuwa baadhi yao husukumwa na umaskini lakini ni nani alisema dawa ya umaskini ni kuiba? Na je, wasipofanikiwa katika uhalifu wanakuwa wamejisaidiaje?

Hebu tuangalie vile ambavyo uhalifu wa aina yeyote ile unavyosababisha hasara chungu nzima. Watu hupoteza maisha yao. Wezi wanapovamia gari na kupora watu huwa ni hasara kubwa sana. Baadhi ya hawa wanaoporwa huwa ni maskini wenye kipato cha chini na kinapoondolewa kuna uwezekana wa familia zao kulalia mate.

Uhalifu mwingine ni ugaidi. Huu ni uhalifu ambao magaidi hulipua majumba makubwa pasi  kujali wala kubali. Huwafanya wengi kulala usingizi usiojua asubuhi. Watu wenye taaluma hujifia tu kama nzige,Waliopuliziwa dawa. Watu huwa ndio kitegauchumi na nchi hupata hasara kubwa sana wanapouliwa.

Nikimalizia, pia kuna wizi wa kalamu. Huu nao ni ufisadi unapoibia serikali pesa, ujue watoto wa maskini watazidi tu kuteseka. Ukiskia kwamba mamilioni ya pesa yameibwa, basi ujue hizo ndizo pesa ambazo zingetumika kusambaza umeme au hata kuleta maji safi karibu nawe.

Nikimalizia uhalifu si lazima uwe ule wa kutumia nguvu peke yake. Uhalifu ni uhalifu na madhara yake ni sawa. Hakuna ule mzuri.

**<u>Maswali</u>**

31. Kwa nini watu wanapoteza matumaini?
A. Visa vya kusafiria vinazidi kuongezeka
B. Uhalifu unazidi kuongezeka
C. Wakenya hawana imani na serikali
D. Uhalifu umeanza kwa kasi

32. Ni ukweli kusema kuwa:-
A. Ni mitaa ya mabanda pekee yenye uhalifu
B. Wahalifu wanapenda kuwashambulia maskini pekee
C. Matajiri pia hushambuliwa na wahalifu
D. Wahalifu wana ubaguzi

33. Kitu kimoja kinachochangia uhalifu ni
   A. Kuiba
   B. Pesa nyingi
   C. Umaskini
   D. Tama ya umaskini
34. Familia kulalia mate ni sawa na familia
   A. Kumeza mate na kulala
   B. Kulala juu ya mate
   C. Kutema mate
   D. Kulala njaa
35. Uhalifu unaohusisha ulipuzi wa majumba huitwa
   A. Ukaidi
   B. Ugaidi
   C. Kifo
   D. kuzirai
36. Usingizi usiojua asubui ni sawa na
   A. ndoto
   B. kiojo
   C. kifo
   D. kuzirai
37. Magaidi
   A. hujali maisha ya watu
   B. hawajali maisha ya watu na mali ya watu
   C. hujali mali ya watu bali si watu
   D. hujali watu tu bila kujali mali yao kama majumba
38. Ni uhalifu gani haujatajwa katika makala
   A. Ufisadi
   B. Uporaji
   C. Kuiba kalamu
   D. Wizi wamali ya umma
39. Kulingana na makala haya, ni huduma gani haziathiriwi na ufisadi?
   A. Umeme
   B. Afya
   C. Maji
   D. Bajeti ya nyumba
40. kichwa mwafaka cha makala haya ni
   A. ufisadi nchini Kenya
   B. uporaji nchini Kenya
   C. ugaidi nchini Kenya
   D. uhalifu nchini kenya

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50***

Otiato alipenda sana kupiga mtindi. Kila wakati alikuwa akienda kwenye baa kutafuta mvinyo ili alewe. Alilewa karibu kila siku. Kutokana na ulevi huu, hakumjali mkewe wala wanawe. Kazi zote nyumbani alizika katika kaburi la sahau. Watu wengi sana waliudhika na tabia yake hii. Ilikuwa aibu kuwaona watoto wa watu wengine wakisoma na wale wa otiato wakizurura tu mashambani kama mbwakoko.

Mara nyingi mkewe alimwonya na kumkaripia. Hata hivyo, yote yalikuwa sawa na kuchota maji kwa pakacha. Alikuwa haambiliki wala hasemezeki. Alikuwa sawa na sikio la kufa ambalo halisikii dawa. Mwenyewe hakuona aibu kuwa ni watoto wake tu walikuwa hawahudhurii masomo. Hakuona aibu kuwa ni nyumbani kwake tu kulikuwa na kelele za kila aina.

Otiato aliendelea kulewa kupindukia . siku moja alipokuwa akitoka katika baa ya karibu huku akipepesuka, alishindwa kabisa kutembea. Hapo alianguka chini kama gunia la viazi. Baada ya kuanguka, usingizi ulimvamia naye akaupokea na kulala fofofo.

Baada ya kulala, wezi walimvamia akiwa usingizini. Walimpora pesa zote zilizokuwa mfukoni. Vilevile waliiba simu yake na kitambulisho chake cha taifa na cha kazi. Hapo akawa amepata funzo la mwaka.

Siku iliyofuata, aliporudi nyumbani alimsimulia bibi yake yote aliyokumbana nayo katika ulevi. Bibi yake hakuwa na la kusema ila kumtupia jicho tu. Kwake huo ulikuwa msiba wa kujitakia ambao hauna kilio. Alijisemea kimoyomoyo, “asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.” Kwa kweli ulimwengu ulimfunza kwa kuwa siku iliyofuata, alikatazwa na askarigongo kuingia kazini pake ati kwa kuwa hakuwa na kitambulisho cha kazi. Baada ya kukosa kuingia kazini, alipigwa kalamu. Hapo akaanza kujuta tabia yake ya ulevi.

41. Kulingana na makala haya KIPAGA MTINDI ni
    A. Kunywa pombe
    B. Kunywa maziwa
    C. Kunywa maji
    D. Kunywa chai
42. Otiato alikuwa na tabia ya
    A. Ambayo ilimfurahisha kila mtu
    B. Iliyoudhi watu wengi
    C. Ya kupendezwa na kuigwa na watu
    D. Ya kumsaidia mkewe na watoto
43. Ni wazi kuwa otiato alikuwa akiishi
    A. Mjini
    B. Katika baa
    C. Baharini
    D. mashambani
44. Ni kweli kusema kuwa
    A. mkewe otiato hakushughulikia tabia za mumewe
    B. mkewe otiato alishughulika kumweleza mumewe abadili tabia
    C. mkewe otiato alikuwa sawa na sikio la kufa
    D. mkewe otiato hakusemezeka wala kuambilika
45. Kupepesuka ni dalili ya
    A. kulewa sana
    B. kutolewa hata kidogo
    C. kuumia miguu kwa jeraha
    D. kukataa kutembea
46. Baada ya kuanguka bwana otiato
    A. hakupata usingizi hata kidogo
    B. alianza kuwatukana wapita njia
    C. alishikwa na usingizi wa mang’amung’amu
    D. alishikwa na usingizi mzito
47. Bwana otiato alikuwa
    A. akifanya kazi bila kulewa
    B. akilewa bila kufanya kazi
    C. akifanya kazi na kulewa
    D. halewi wala hafanyi kazi
48. Kulingana na bibi yake , otiato
    A. hakustahili kufutwa kazi
    B. alijitakia shida alizozipata yeye mwenyewe
    C. alikuwa mtu mzuri mwenye kupendwa na kila mtu
    D. alistahili kupandishwa kazi
49. Funzo la kisa hiki ni
    A. kunywa pombe kupita kiasi si hatia
    B. ulevi ni mbaya
    C. kulewa kidogo si hatia
    D. ulevi si mbaya sana
50. Sikio la kufa ni

A. mtu anayesikia mawaidha
B. mtu asiyesikia mawaidha
C. mtu anayewatukana wengine
D. mtu anayewapenda wengine